# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA

## BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU TANZANIA (NBAA)

SIMU: +255 26 2963318-9;
NUKUSHI: +255 22 2150648
BARUA PEPE: info@nbaa.go.tz
TOVUTI: www.nbaa.go.tz

4 BARABARA YA UKAGUZI,
"JENGO LA UKAGUZI", GHOROFA YA NANE,
S.L.P. 1271,
41104 TAMBUKARELI,
**DODOMA, TANZANIA**

Unapojibu tafadhali taja:
**Kumb. Na.:** DE.17/367/01/31

**Tarehe:** 21 Desemba 2023

**TAARIFA KWA UMMA**

**MATOKEO YA MITIHANI YA 98 YA NBAA ILIYOFANYIKA NOVEMBA 2023 PAMOJA NA UZINDUZI WA MIHUTASARI MIPYA YA MITIHANI YA NBAA NA VITABU VYA REJEA**

## 1.0 Utangulizi

Bodi ya Wakurugenzi ya NBAA katika kikao chake cha kwanza kilichofanyika leo tarehe 21.12.2023 chini wa Mwenyekiti wake CPA.Prof. Sylvia S. Temu, kimeidhinisha matokeo ya mitihani ya 98 ya Bodi kwa watahiniwa waliofanya mitihani ya hiyo iliyofanyika mwezi Novemba 2023.

Mitihani hiyo ilifanyika katika vituo kumi na viwili vya mitihani vilivyopo Tanzania Bara na Visiwani. Mitihani hiyo ilihusisha watahiniwa katika hatua ya Kwanza na ya Pili katika Ngazi ya Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC I, ATEC II) zenye masomo manne kila moja na Ngazi ya Taaluma; Hatua ya Msingi (Foundation Level) yenye masomo sita, Hatua ya Kati (Intermediate Level) yenye masomo sita na Hatua ya Mwisho (Final Level) yenye masomo manne. Mitihani hii ni ya kumi na tisa chini ya mfumo mpya wa elimu na mafunzo unaozingatia weledi.

## 2.0 Matokeo ya mitihani

### 2.1 Matokeo ya Jumla

Watainiwa waliosajiliwa walikuwa **7,238.** Watahiniwa **527** sawa na asilimia **7.3** hawakuweza kufanya mitihani kwa sababu mbalimbali. Hivyo idadi ya watahiniwa waliofanya mitihani hiyo ni **6,711** sawa na asilimia **92.7**. Kati ya watahiniwa walisajiliwa kufanya mitihani watahiniwa **3,636** sawa na asilimia **50.2** walikuwa wanawake na watahiniwa **3,602** sawa na asilimia **49.8** walikuwa wanaume.

Kati ya watahiniwa waliofanya mitihani hiyo watahiniwa **4,468** sawa na asilimia **66.6** wamefaulu mitihani yao ambao kati yao watahiniwa **1,185** sawa na asilimia **17.7** ni wale waliofaulu masomo yote katika ngazi husika na hivyo wanastahili kupatiwa barua za ufaulu na watahiniwa **3,283** sawa na asilimia **48.9** ni watahiniwa ambao wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi husika. Watahiniwa waliobakia ambao ni **2,243** sawa na asilimia **33.4** walishindwa mitihani yao katika ngazi husika.

| MUHULA WA MITIHANI | WALIOSAJILIWA (No & %) | WALIOFANYA (No & %) | WALIOFAULU | | WALIOSHINDWA (No & %) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | WALIOFAULU MASOMO YOTE (No & %) | WALIOFAULU BAADHI YA MASOMO (No & %) | |
| Novemba 2022 | 6,429 | 5,910 (91.9) | 1,303 (22.0) | 2,691 (45.6) | 1,916 (32.4) |
| Novemba 2023 | 7,238 | 6,711 (92.7) | 1,185 (17.7) | 3,283 (48.9) | 2,243 (33.4) |

Kwa mantiki hiyo asilimia ya ufaulu katika muhula huu wa Novemba 2023 ambayo ni 66.6 imeshuka kwa asilimia moja ukilinganisha na muhula sawa na huu wa Novemba 2022 ambapo asilimia ya ufaulu ilikuwa 67.6.

## 2.2 Watahiniwa waliofaulu kutunukiwa Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC) na Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA)

### 2.2.1 Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC)

Jumla ya watahiniwa **53** wamefaulu mtihani wa Ngazi ya Cheti (Accounting Technician Level II). Kati ya watahiniwa hao wanawake ni **25** sawa na asilimia **47.2** na wanaume ni **28** sawa na asilimia **52.8.** Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya Cheti kufikia **4,275** tangu mitihani hii ianze mwaka 1991.

### 2.2.2 Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA)

Jumla ya watahiniwa **236** wamefaulu mtihani wa Shahada ya Juu ya Uhasibu nchini - CPA (T). Kati ya watahiniwa hao wanawake ni **129** sawa na asilimia **54.7** na wanaume ni **107** sawa na asilimia **45.3.** Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya CPA kufikia **12,888** tangu mitihani hii ianze mwaka 1975.

### 2.2.3 Vyuo Bora

Kati ya watahiniwa 236 waliofuzu kutunukiwa Cheti cha Taaluma ya Juu ya Uhasibu [CPA(T)], wengi wao wametoka katika vyuo vifuatavyo: watahiniwa **56** sawa na asilimi **23.6** wametoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, watahiniwa **46** sawa na asilimia **19.4** wametoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha, watahiniwa **39** sawa na asilimia **16.5** wametoka Chuo Kikuu Mzumbe, watahiniwa **15** sawa na asilimia **6.3** wametoka Chuo cha Uhasibu Tanzania na watahiniwa **13** sawa na asilimia **5.5** wametoka Chuo cha Uhasibu Arusha.

### 2.2.4 CPA (T) Linganifu [(CPA(T)] Equivalent

Jumla ya watahiniwa **10** wamefaulu mtihani wa CPA (T) Linganifu [(CPA (T)] Equivalent Qualification. Kati yao **04** sawa **40.0** ni wanamke na watahiniwa **06** sawa na asilimia **60.0** ni wanaume. Jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani hii sasa imefikia **296** tangu mitihani hii ianze Novemba 2014.

## 2.3 Matokeo katika Ngazi Mbalimbali

### 2.3.1 Ngazi ya Cheti (Accounting Technician)

#### 2.3.1.1 Hatua ya Awali ya Cheti (Accounting Technician Level I)

Katika ngazi ya awali ya mitihani ya Uandishi na Utunzaji wa Hesabu (ATEC I) watainiwa waliosajiliwa walikuwa 107 kati ya hao watahiniwa **06** sawa na asilimia **5.6** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **101** sawa na asilimia **94.4**.

Kati ya watahiniwa **101** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **77** ambao ni asilimia **76.2** wamefaulu mitihani mitihani yao. Kati yao watahiniwa **44** sawa na asilimia **43.5** wanastahili kutunukiwa Barua za Ufaulu na watahiniwa **33** sawa na asilimia **32.7** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi husika. Watahiniwa waliobakia **24** sawa na asilimia **23.8** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.1.2 Hatua ya Pili ya Cheti (Accounting Technician Level II)

Katika ngazi ya pili ya mitihani ya Uandishi na Utunzaji wa Hesabu (ATEC II) watainiwa waliosajiliwa walikuwa **206** kati ya hao watahiniwa **13** sawa na asilimia **6.3** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **193** sawa na asilimia **93.7**.

Kati ya watahiniwa **193** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **146** ambao ni asilimia **75.6** wamefaulu mitihani mitihani yao. Kati yao watahiniwa **54** sawa na asilimia **27.9** wanastahili kutunukiwa Barua za Ufaulu na watahiniwa **92** sawa na asilimia **47.7** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi husika. Watahiniwa waliobakia **47** sawa na asilimia **24.4** hawakufaulu mitihani yao.

### 2.3.2 Ngazi ya Taaluma (Professional Stage)

#### 2.3.2.1 Hatua ya Awali (Foundation Level)

Katika ngazi ya awali ya taaluma (Foundation Level) watainiwa waliosajiliwa walikuwa **973** kati ya hao watahiniwa **83** sawa na asilimia **8.3** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **890** sawa na asilimia **91.5**.

Kati ya watahiniwa **890** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **741** ambao ni asilimia **83.3** wamefaulu mitihani mitihani yao. Kati yao watahiniwa **290** sawa na asilimia **32.6** wanastahili kutunukiwa Barua za Ufaulu na watahiniwa **451** sawa na asilimia **50.7** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi husika. Watahiniwa waliobakia **149** sawa na asilimia **16.7** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.2.2 Hatua ya Kati (Intermediate Level)

Katika ngazi ya kati ya taaluma (Intermediate Level) watahiniwa waliosajiliwa walikuwa **3,913** kati ya hao watahiniwa **308** sawa na asilimia **7.9** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **3,605** sawa na asilimia **92.1**.

Kati ya watahiniwa **3,605** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **2,435** ambao ni asilimia **67.5** wamefaulu mitihani mitihani yao. Kati yao watahiniwa **557** sawa na asilimia **15.4** wanastahili kutunukiwa Barua za Ufaulu na watahiniwa **1,878** sawa na asilimia **52.1** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi husika. Watahiniwa waliobakia **1,170** sawa na asilimia **32.5** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.2.3 Hatua ya Mwisho (Final Level)

Katika ngazi ya mwisho ya taaluma (Final Level) watainiwa waliosajiliwa walikuwa **2,039** kati ya hao watahiniwa **117** sawa na

asilimia **5.7** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **1,922** sawa na asilimia **94.3**.

Kati ya watahiniwa **1,922** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **1,069** ambao ni asilimia **55.6** wamefaulu mitihani mitihani yao. Kati yao watahiniwa **404** sawa na asilimia **12.5** wanastahili kutunukiwa Barua za Ufaulu na watahiniwa **829** sawa na asilimia **43.1** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi husika. Watahiniwa waliobakia **853** sawa na asilimia **44.4** hawakufaulu mitihani yao.

**3.0 Pongezi**

Bodi inawapongeza wale wote waliofuzu mitihani yao na kuwataka wale ambao hawajafuzu kutokata tamaa bali waongeze bidii zaidi katika masomo yao ili waweze kufanya vizuri katika mitihani ijayo ya Bodi. Bodi inawashauri kutumia vema vitabu vilivyotayarishwa na Bodi katika kijiandaa kwa mitihani yao. Pia wanashauriwa kusoma vitabu vingine vya ziada ili kuongeza ufahamu zaidi katika masomo hayo.

**4.0 Mitihani inayofuata**

**4.1 Mitihani ya katikati ya mihula:**

- **Februari 2024:** Jumatatu tarehe 19 hadi Ijumaa tarehe 23 February 2024
- **Agosti 2024:** Jumatatu tarehe 19 hadi Ijumaa tarehe 23 Agosti

**4.2 Mitihani ya Mihula mikubwa**

- **Mei 2024:** Jumanne tarehe 30 April hadi Ijumaa tarehe 3 Mei 2024
- **Novemba 2024:** Jumanne tarehe 5 hadi Ijumaa tarehe 8 Mei 2024

**4.3 Mapitio ya Mitaala ya Bodi pamoja na vitabu**

4.4 Tunapenda kuwafahamisha watahiniwa pamoja na umma wote kwa ujumla kuwa Bodi imekamilisha zoezi la kupitia mitaala yake pamoja na vitabu vya kiada ambavyo vitakuwa tayari kwa matumizi kuanzia Januari 2024. Mitihani ya kwanza kwa Mihtasari hii mipya pamoja na vitabu vyake itafanyika kuanzia mwezi Novemba 2024.

Matokeo haya ya mitihani ya **98** ya Bodi yanapatikana katika tovuti ya NBAA ambayo ni **www.nbaa.go.tz**

**UZINDUZI WA MIHUTASARI MIPYA YA BODI PAMOJA NA VITABU VYA REJEA**

**Utangulizi:** Bodi ilianza mchakato wa kupitia mitaala yake pamoja na vitabu vya rejea kuanzia mwezi Agosti 2022. Lilianza kwanza zoezi la marekebisho ya mitaala na baada ya kumalizika zoezi la kupitia vitabu vya rejea lilifuatia. Bodi hufanya mapitio ya mitaala yake pamoja na vitabu kila baada ya miaka mitano. Zoezi la mwisho lifanyika mwaka 2019. Bodi inayo mihtasari (syllabi) mitatu ambayo ni Mtaala wa Cheti Ngazi ya Awali (Accounting Technician Level I) ambao una masomo manne; muhutasari wa pili ni wa wa Cheti Ngazi ya Pili (Accounting Technician II) ambao pia una masomo manne; muhutasari wa tatu ni ule wa Ngazi ya Taaluma (Professional Level) ambao una masomo kumi na sita. Hivyo idadi ya masomo katika mihtasari yote mitatu ni ishirini na nne.

**Kazi iliyofanyika:** kazi ya kurekebisha mihtasari ilianza kwanza na zoezi la kuchukua maoni kutoka kwa wadau mbalimbali. Baada ya kukusanya maoni hayo yalichakatwa na kutumika kama nyenzo mojawapo katika zoezi la mapitio. Lilifuta zoezi la kupitia somo moja baada ya jingine ili kuondoa mada zilizokuwa zimepitwa na wakati na kuingiza mada mpya. Pia kuongeza mada mpya ambazo hazikuwepo kabisa. Kumekuwepo na maboresho kwenye kila somo japo kuna baadhi ya masomo ambayo yaliboreshwa kwa kuongezewa mada za somo jingine. Mfano somo la Uchumi liliongezewa mada za Kodi na somo la Uhasibu liliongezewa mada za Ukaguzi. Masomo yote haya yapo kwenye Ngazi ya Awali ya Taaluma. Baada ya maboresho ya mihutasari lilifuatia zoezi la marekebisho ya vitabu vya rejea. Zoezi hili lilihakikisha kwamba kila mada iliyopo kwenye Mihutasari inayo notisi za rejea kwenye kitabu.

**Kuanza kutumika:** Mihtasari mipya pamoja na vitabu vya rejea vitaanza kutumika kuanzia Januari 2024 ila mitahani ya kwanza itafanyika mwezi wa Novemba 2024.

**Pongezi:** Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Uongozi mzima wa NBAA unapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wataalamu wote walioisaidia Bodi katika zoezi zima la kupitia mitaala yake pamoja na vitabu vya rejea. Bodi itendelea kutambua mchango wao katika taaluma nzima ya Uhasibu hapa nchini.

**Mwito:** Bodi inatoa wito kwa Watahiniwa wote wa Mitihani ya Bodi waliopo na watakaosajiliwa baadae pamoja na Walimu kutumia mitaala hiyo pamoja na vitabu vya rejea kwa usahihi ili kuongeza ufaulu katika mitihani ya Bodi.

**Mwisho:** Sasa naomba kutangaza rasmi kuwa mihtasari mipya ya mitihani ya Bodi pamoja na vitabu vya rejea vimezinduliwa rasmi leo tarehe 21.12.2023.

**ASANTENI**

**CPA. PIUS A. MANENO**
**MKURUGENZI MTENDAJI**